## HATUA ZA
# KUJISAJILI

**1**
**INGIA** KWENYE TOVUTI
WWW.INVEST.LOREAL.COM

**2**
**BOFYA**
KITUFE CHA "SAJILI"

**3**
**INGIA** NA JINA LAKO LA MTUMIAJI NA NENOSIRI

**4**
**FANYA UCHAGUZI WAKO**
KWA KUKAMILISHA SKRINI YA USAJILI

**5**
**USISAHAU KUTHIBITISHA**
USAJILI WAKO

USAJILI WA CHINI → **HISA 1 YA L'ORÉAL**

USAJILI WA JUU → **HISA 50 ZA L'ORÉAL[3]**

KIASI CHA 25% YA FIDIA YAKO YA UJUMLA YA MWAKA WA 2020

[3] *Iasi hiki kinaweza kupunguzwa katika tukio la usajili wa idadi kubwa kupita kiasi.*

OEB_FCPE_HZE_KEN_SWA20 - Mikopo ya picha: Shutterstock - GettyImages

L'ORÉAL

WWW.INVEST.LOREAL.COM

UTOAJI KWA UFUPI

## MPANGO WA UMILIKI WA HISA KWA WAAJIRIWA 2020





TAREHE 17 SEPTEMBA HADI TAREHE 2 OKTOBA 2020

# NASEMA





# NDIYO!

L'ORÉAL

WWW.INVEST.LOREAL.COM

## YOTE YA KUFAHAMU KUHUSU MPANGO WA UMILIKI WA HISA KWA WAAJIRIWA

L'Oréal inakupa fursa nyingine ya kujihusisha na maendeleo ya Kundi kwa kuwa mwanahisa kupitia "Hazina ya Uwekezaji wa Kampuni" "Mpango wa Hisa kwa Waajiriwa wa L'Oréal".

Hazina ya Uwekezaji wa Kampuni "Mpango wa Hisa kwa Waajiriwa wa L'Oréal" ni mfuko wa pamoja unaohifadhiwa kwa waajiriwa wa Kundi wanaotaka kuwekeza katika hisa za L'Oréal.

**Kwa kushiriki katika Mpango huu mpya wa umiliki wa hisa kwa waajiriwa, unaweza kununua hisa za L'Oréal kwa masharti ya upendeleo.**

Kipunguzo **cha 20%** kwenye bei ya rejeo * ya hisa

Mchango wa mwajiri hadi **hisa 4 zinazotolewa na L'Oréal** kulingana na uwekezaji wako

Uwezekano wa kulipa kwa uhawilisho wa benki na/au malipo 12 ya kila mwezi yanayoondolewa kwa mshahara

### KUMBUKA KABLA YA KUWEKEZA

**Mwishoni mwa ushiriki wako katika Mpango, utakuwa mwanahisa wa L'Oréal**
Kwa hivyo, utapokea gawio lolote litakalolipwa kila mwaka ambalo litawekezwa katika FCPE. Gawio hili litaongezeka kwa 10% baada ya miaka miwili ya kalenda ya umiliki wa hisa zako, yaani mwaka 2023.
Kama mwanahisa yeyote, uwekezaji wako utafuatia mageuzi ya bei ya hisa ya L'Oréal inapoenda juu na pia chini. Kwa hiyo kuna hatari ya kupoteza mtaji.

**Thamani ya uwekezaji wako inatofautiana na mabadiliko katika viwango vya ubadilishaji**
Kwa kuwa hisa za L'Oréal zimeorodheshwa katika yuro kwenye soko la hisa la Paris, wakati wa uwekezaji wako; thamani ya uwekezaji wako itatofautiana kwa mujibu wa kupanda na kushuka kwa kiwango cha ubadilishaji kati ya yuro na sarafu yako.

**Uwekezaji wako umezuiwa kwa miaka 5**
Uwekezaji wako umezuiwa hadi tarehe 3 Novemba 2025, isipokuwa ikiwa utatolewa mapema.

** Bei ya rejeo ni wastani wa bei za ufunguzi za hisa ya L'Oréal zitakazotumiwa kati ya tarehe 17 Agosti na tarehe 11 Septemba 2020 na itawekwa tarehe 14 Septemba 2020.*

## KANUNI YA MCHANGO WA MWAJIRI

Kama sehemu ya Mpango wa umiliki wa hisa kwa waajiriwa, mchango wa mwajiri utalipwa kulingana na gridi ya hapa chini:

| Ukinunua katika mwaka wa 2020 idadi ya hisa sawa na: | + Mwaka wa 2025, L'Oréal inakupa hisa za ziada sawia na: | = Jumla ya uwekezaji wako katika 2025: |
|---|---|---|
| **1** | **1** | hisa **2** |
| **2** | **1** | hisa **3** |
| **3** | **2** | hisa **5** |
| **4** | **2** | hisa **6** |
| **5** | **2** | hisa **7** |
| **6** | **2** | hisa **8** |
| **7** | **3** | hisa **10** |
| **8** | **3** | hisa **11** |
| **9** | **3** | hisa **12** |
| **10** na zaidi[1] | **4** | hisa **14** na zaidi |

*Zaidi ya hisa 10 zilizosajiliwa, mchango unabakia kwa hisa 4.*

### MFANO

**Chukulia bei ya kumbukumbu ya hisa ya L'Oréal kuwa 250 €. Bei ya ununuzi wa hisa yako itakuwa 200 € (yaani 250 € baada ya kuondoa kipunguzo cha 20%).**

Unataka kununua hisa 3

Mnamo 2020,
unalipia hisa 3 kwa bei ya kipunguzo,
yaani **600 €** (200 € x 3)

+

**Mnamo 2025, L'Oréal inakupa hisa 2.**
Chukulia kwamba bei ya hisa ya L'Oréal ni **250 €** katika mwaka wa 2025.

→ Thamani ya uwekezaji wako mwaka wa 2025 ni **1,250 €** (5 x 250 €)

Katika mfano huu, unapata faida kubwa ya **650 €**[2]

*[1] Idadi ya hisa ambazo unaweza kununua ni kiasi cha hisa 50 (isipokuwa katika usajili wa idadi kubwa kupita kiasi).*
*[2] Ukiondoa kodi na gawio lolote.*

## NI NANI ANAWEZA KUJISAJILI?

Mwajiriwa yeyote atakayekuwa amedumu angalau kwa miezi 24 ifikapo tarehe 2 Oktoba 2020.

## NI NINI KITAFANYIKA BAADA YA KUJISAJILI?

**Hisa zako katika hazina zinafungwa kwa miaka 5 ,** hivyo huwezi kuziuza kabla ya mwisho wa kipindi cha kufunga. Hata hivyo, matukio fulani ya kutolewa mapema yanaonekana kama ilivyoelezwa kwenye hati **"Local Supplement".**

**Hifadhi inayotolewa kwenye mchango wa mwajiri,** itawasilishwa kwako mwishoni mwa kipindi cha kuzuia, karibu tarehe 3 Novemba 2025. Hizi hisa za bonasi zitawasilishwa kwako ikiwa wewe ni mfanyakazi wa Kundi la L'Oréal katika tarehe hiyo (isipokuwa nyakati zilizotajwa katika "Sheria za PAGA").

**Ada ya matengenezo ya akaunti imegharamiwa na L'Oréal.**

**INGIA KUPITIA**
WWW.INVEST.LOREAL.COM

- Kwa maelezo zaidi juu ya utoaji huu
- Kwa kutekeleza mizandiki ya uwekezaji
- Kwa kujisajili kuanzia tarehe 17 Septemba hadi tarehe 2 Oktoba 2020